

USAFIRISHAJI



Mabasi ya Kampuni ya ABC Class yakiwa yameegeshwa kwenye ofisi zake zilizopo Manzese jijini Dar es Salaam, yakisubiri kuanza safari. Picha na Michael Matemanga

Taboa, wananchi waona ugumu mabasi kurejea Stendi ya Magufuli

Devotha Kihwelo na Nasra Abdalla, Mwananchi
mwananchinews@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Zikiwa zimesalia siku tatu kabla ya kuanza kutekelezwa kwa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chamila la kutaka mabasi yandayo mikoani yanayopakia na kushusha abiria nje ya Kituo cha Mabasi cha Magufuli kurejea kituoni hapo, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Yaendayo Mikoani (Taboa) kimeeleza ugumu katika utekelezaji.

Agosti 11, 2026, Chalamila aliziagiza kampuni za mabasi kurejea Kituo cha Magufuli ifikapo Jumatatu wa wiki ijayo, isipokuwa sita zilizo na vibali maalumu kutoka Mam-laka ya Udhambi Usafiri Ardhi-ni (Latra).

Akizungumza na Mwananchi juzi, Katibu wa Taboa, Priscus Joseph alisema yapo mambo kadhaa yanayolifanya agizo hilo kuwa gumu kati-ka kutekelezeka, licha ya mat-amko mbalimbali yaliyowahi kutolewa.

Joseph alisema moja ya changamoto ni mpangilio wa miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, ambayo ofisi nyingi za kampuni za mabasi zipo nje ya Wilaya ya Ubungo ilipo Stendi ya Magufuli.

Alisema mabasi yanap-awasogeza abiria mjini kuto-ka maeneo ya pembezi, huwasaidia na huwa hawa-tozwi nauli ya ziada kwa huduma hiyo.



Mabasi ya Kampuni ya Ratco yakiwa yameegeshwa kwenye ofisi za kampuni hiyo zilizopo Magomeni Kagera Jijini Dar es Salaam jana, yakisubiri kuanza safari. Picha na Michael Matemanga

"Sasa hivi pale Magufu-li usiku hakuna usafiri wa mwendokasi. Unategemea abiria apande nini, hasa aki-wa na mizigo yake? Unamwa-chaje abiria katika mazingira hayo ndani ya kituo?" alihoji Joseph.

Jambo jingine ni usafirish-aji wa mizigo, ambalo Joseph alisema kampuni nyingi zin-azotoa huduma za mizigo bandarini zina ofisi zake mji-ni, kama ilivyo kwa Bandari ya Dar es Salaam na kituo cha SGR, vyote vikiwa katikati ya mji.

Alisema hali hiyo inafan-ya iwe vigumu kwa kampuni kupeleka mizigo yote Stendi ya Magufuli, hasa inayoweza kufikia tani mbili.

Hoja ya msongamano

Akizungumzia hoja kwam-ba mabasi hayo yanasaba-bisha msongamano mjini,

Joseph ameipinga akisema foleni za barabara za Jiji la Dar es Salaam haziwezi kuhu-sishwa na mabasi pekee.

"Barabara ya Mandela ime-kithiri kwa foleni, je, mabasi yanahusika?" alihoji.

Alisema walikubaliana mabasi yote yawe yanapi-ta Magufuli kwa ukaguzi na kulipia mapato, lakini kuna baadhi ya magari hata yan-ayopita Bagamoyo hayapiti.

Alisema badala ya kuondoa mabasi kwenye stendi binafsi, Joseph alipendekeza viwe-kwe viziuzi katika Barabara ya Bagamoyo ili magari yan-ayopita huko yapitite Sten-di ya Magufuli kwa ajili ya ukaguzi.

Alisema ukaguzi huo unaweza kusaidia kudhibiti usafirishaji wa bidhaa zisizo halali, dawa za kulevya, kemi-kali pamoja na masuala ya uhamiaji.

Akizungumzia kampuni zilizopewa vibali maalumu kutumia stendi binafsi, Joseph alisema anachofaha-mu zipo 11 na si sita kama zilivyotajwa na mkuu wa mkoa na akasisitiza kuwa Taboa itaendelea kuzilinda kampuni hizo.

"Wewe unampa mtu kibali, anajenga stendi ya Sh2 bili-oni, halafu leo unamwambia kibali kimeisha aondoke. Hilo jengo atafanyia nini? Hii ni kuchezea mitaji ya watu," alisema.

Alisema leseni huende-lezwa kila mwaka, lakini mwekezaji hawezi kurejesha mtaji wa Sh2 bilioni ndani ya mwaka mmoja.

Wananchi wagawanyika

Baadhi ya wananchi walio-zungumza na Mwananchi kuhusu amri hiyo, wame-pinga abiria kulazimishwa

kupanda au kushuka Stendi ya Magufuli, wakisema hatua hiyo inaweza kuwaongezea gharama za usafiri.

Rose Marco, mkazi wa Chanika, alisema safari ya kuifikia Stendi ya Magufuli inaweza kumgharimu zaidi ya Sh20,000, fedha ambazo angeziokoa aki-pandia basi Chanika.

Naye Maelo Herman, mka-zi wa Magomeni, alisema kwa abiria anayeenda mkoani aki-wa na mizigo, ili aifikie Stendi ya Magufuli atajikuta anatumia fedha nyingi kuliko hata nauli ya kwenda mkoani.

Naye Mwantumu Ibrahim alisema mabasi yanayopakia abiria katika maeneo ya pem-bezoni yana msaada mkubwa kutokana na foleni zisizota-birika jijini, hivyo badala ya kuyaondoa, Serikali iweke utaratibu wa kuyasimamia.

Kwa upande wake, wakala wa mabasi katika Stendi ya Magu-fuli, Justine Haule alisema hapigani na uamuzi wa mkuu wa mkoa, isipokuwa anashauri utekelezaji uwe wa usawa kwa kampuni zote.

Halmashauri yalia hasara

Katikati ya malalamiko hayo, Ofisa Habari na Uhusiano wa Manispaa ya Ubungo, Joia Nzali alisema halmashauri hiyo inapata hasara kutokana na mabasi kutotumia Stendi ya Magufuli.

Alisema awali, wakati Stendi ya Ubungo ikiwa imezidiwa na wingi wa mabasi, Latra ilitoa vibali vya muda kwa baadhi ya kampuni, lakini havijawahi kubatilishwa hata baada ya kukamilika ujenzi wa Stendi ya Magufuli.

Alisema ukosefu huo wa mapato umeathiri ujenzi wa kituo hicho, ambao ulipangwa kufanyika kwa awamu tatu.

Latra na utekelezaji

Licha ya kelele kuhusu sua-la hilo, Kaimu Meneja Udhibiti magari ya abiria Latra, Ngere-za Patel alisema wamejipanga kuanza ufuatiliaji na utekeleza-ji wa maelekezo na Chalami-la, kuhakikisha mabasi yote walioyapa leseni yanaishia kwenye maeneo ambayo leseni zake zinasoma.

"Tunapotoa leseni kwa basi lolote tunalipa ratiba na ina-onyesha uanzie safari kwenye kituo gani na uishie kituo gani," alisema Patel.

Alisema katika Mkoa wa Dar es Salaam mabasi yanayotoka kanda za Kaskazini, kati, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini yana-ishia kwenye Kituo cha Magu-fuli na yale ya Kusini yanaishia Mbagaji.

Alisema hakuna kituo cho-chote ambacho wameruhusu mabasi hayo yaweze kugesh-wa na kwa mujibu wa leseni zao wanatakiwa wafuate utara-tibu ambao upo, ambao ni moja wapo ya masharti ya leseni zao.

Alisema baada ya tarehe zilizopangwa na mkuu wa mkoa kuisha, watachukua hat-ua kwa wale wote watakaoki-uka taratibu waliopatiwa kwa mujibu wa leseni zao.

"Sasa hivi pale Magufu-li usiku hakuna usafiri wa mwendokasi. Unategemea abiria apande nini, hasa akiwa na mizigo yake? Unamwa-chaje abiria katika mazingira hayo ndani ya kituo?"

Priscus Joseph

HABARILEO JUMAMOSI AGOSTI 15, 2022

Latra yawaita wawekezaji wa daladala Ilemela

Na Alexander Sanga, Mwanza

MAMLAKA ya Udhubiti Usafiri Ardhi (LATRA) imewahamasisha wawekezaji wa huduma za daladala kuwekeza katika njia mbalimbali katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuboresha upatikanaji wa huduma za usafiri kwa wananchi.

Akizungumza jana katika mahojiano maalumu jijini Mwanza, Ofisa Leseni na Usajili wa Latra Mkoa wa Mwanza, Steven Kusupa alisema njia ya daladala kutoka Mwanza mjini hadi Hospitali ya Wilaya ya Ilemela tayari imeanzishwa lakini bado hakuna watoa huduma wa kutosha wanaoendesha magari katika njia hiyo.

Alisema Latra inaendelea kuhamasisha wawekezaji kupeleka magari katika njia hiyo na kuwataka wadau, wakiwemo viongozi wa serikali na wananchi, kushiriki kuvutia uwekezaji ili huduma hiyo ianze kutolewa kwa ufanisi. Kusupa alisema kuhusu njia ya mzunguko kutoka Lumala kupitia Greenview hadi Kiseke PPF, kuwa njia hiyo tayari ilianzishwa lakini hadi sasa hakuna mwombaji wa leseni ya kuendesha huduma za usafiri katika eneo hilo.

Alieleza kuwa mamlaka yao imeanza kukusanya maoni kutoka kwa wadau, kubaini namna bora ya kuchochea uwekezaji utakaowezesha huduma kuanza kutolewa katika njia hiyo.

Aidha, alisema mamlaka tayari imeanzisha njia ya Kisesa kupitia Ndama, Busenga, Buswelu na Kiseke PPF hadi Mwaloni na imeshaitangaza kwa wadau, huku ikiendelea kuwakaribisha waombaji wa leseni za uendesaji wa daladala.

Akizungumzia kuhusu malalamiko ya magari ya daladala ya njia ya Mwaloni-Lukobe kutofika mwisho wa safari na kuishia eneo la Roundabout ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Kusupa amesema changamoto hiyo ilisababishwa na ubovu wa barabara na mwikio mdogo wa abiria waliokuwa wakipendelea kutumia boda-boda au kutembea kwa miguu.

Alisema Latra imechukua hatua za kiudhibiti dhidi ya magari yanayokatisha njia na sasa imeanza utekelezaji wa utaratibu wa kufunga vifaa vya ufuatiliaji wa mwenendo wa magari (GPS) kwa daladala zinazobainika kukiuka masharti hayo, huku baadaye utaratibu huo ukihusisha pia magari yote yatakayokuwa yakihushia leseni zao za njia za safari.

Vilevile, amewaomba wananchi kuendelea kutoa taarifa za ukiukwaji wa masharti ya utoaji huduma ili kuboresha usafiri wa umma na kuhakikisha magari yanazingatia njia zilizoidhinishwa.